**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA MHESHIMIWA BAHAME T. NYANDUGA, KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU KUHUSU MIKAKATI YA KUKOMESHA MAUAJI NA UKATILI DHIDI YA WATU WENYE ULEMAVU WA NGOZI , TAREHE 18/ 03/2015 KATIKA OFISI ZA TUME YA HAKI ZA BINADAMU**

***Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,***

***Waheshimiwa wawakilishi wa Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia (AZAKI),***

***Waheshimiwa Viongozi wa Dini,***

***Ndugu wanahabari,***

***Washiriki wote,***

***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za Asubuhi.***

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia afya na uhai na kutukutanisha hapa leo. Pili, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwenu nyie kwa kuitika wito wetu na kufika katika kikao hiki muhimu ili kujadili mpango mkakati wa kudumu kwa madhumuni ya kukomesha vitendo vya kikatili vya uvunjifu wa haki za binadami kwa watu wenye ulemavu wa ngozi.

**Ndugu washiriki,**

Sisi katika Tume, kama watanzania wengine kote nchini, tumeguswa na kusikitishwa na matukio ya hivi karibuni, hasa mauaji ya mtoto Yohana Bahati na kukatwa na kujeruhiwa vibaya mama yake Ester Jones, na pia kukatwa kiganja mtoto Baraka Cosmas na kujeruhiwa mama yake Prisca Cosmas, matukio ambayo tunayalaani.

Lengo kubwa la kukutana kwetu hapa leo ni kujadili na kupanga mkakati wa kitaifa wa kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu hasa haki za watu wenye ulemavu wa ngozi pamoja na kutafuta mbinu au mkakati endelevu wa kutokomeza mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Ni ukweli usiopingika kwamba vitendo vinavyoendelea dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi ni vya ukatili uliokithiri, vinavyohuzunisha, kufadhaisha na kufedhehesha ndani na nje ya mipaka ya Tanzania. Hali hii inawanyima ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi haki ya kuishi (right to life), haki ya kutoteswa (freedom from torture) na haki ya usalama wa mtu (right to security of person) – haki ambazo ni za msingi sana kwa binadamu.

**Ndugu washiriki,**

Haki ya kuishi imeainishwa katika Katiba yetu ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kimataifa na ya kikanda ambayo Tanzania imeridhia ikiwamo:.

- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 (International Covenant on Civil and Political Rights) umebainisha haki ya kuishi katika Ibara 6.

- Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 (African Charter on Human and Peoples' Rights) umeelezea haki hii ya kuishi kupitia Ibara ya 4.

- Tanzania pia imeridhia mikataba mingine inayolinda haki za watoto na haki za wanawake ambao ndio waathirika wakuu wa janga hili la kitaifa.

Ni jambo la kusikitisha kwamba pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali na wadau wengine, bado kumekuwa na changamoto kubwa katika kuhakikisha haki ya kuishi kwa ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi inalindwa na pia kupata hifadhi stahiki kutoka kwa wanajamii na serikali. Changamoto hii ndiyo inatufanya tukutane hapa leo ili tushauriane namna gani bora ya jinsi tutakavyochangia kulingana na nafasi aliyonayo kila mmoja wetu jitihada za kukomesha mauaji na ukatili kwa watu wenye ulemavu wa ngozi.

Katika matukio ya hivi karibuni, watoto wamekuwa wakilengwa zaidi katika ukatili huu.

Tarehe 15 Februari 2015, mtoto **Yohana Bahati** mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu, alichukuliwa kwa nguvu nyumbani kwao na watu wasiojulikana wakiwa wamebeba silaha mkoani Geita na mwili wa mtoto ulionekana baada ya siku mbili kilometa chache kutoka nyumbani kwako, akiwa amekatwa mikono na miguu yote.

Tarehe 6 Machi 2015, mtoto mwingine aitwae **Baraka Cosmas** mwenye umri wa miaka sita akiwa amelala nyumbani usiku na mama yake katika kijiji cha Kipenda, mkoani Rukwa, alivamiwa na kundi la watu wasiojulikana ambao walimkata mtoto huyo kiganja chake cha mkono wa kulia na kutoweka nacho. Mtoto huyo na mama yake ambaye pia alijeruhiwa katika harakati hizo wanaendelea kupata matibabu mkoani Mbeya.

Pia mtoto **Pendo Emmanuel** mwenye umri wa miaka minne aliibiwa katika mazingira ya kutatanisha Januari 2015 nyumbani kwao mkoani Mwanza. Bado mtoto huyo hajapatikana hadi leo jambo ambalo linahuzunisha na kutia simamzi kubwa kwa wanafamilia na Watanzania kwa ujumla.

Haya ni matukio ya kusikitisha, ya kikatili na kinyama.

Tangu mwaka 2006 hadi sasa, takribani watu 70 wenye ulemavu wa ngozi wameshauawa na wangine kujeruhiwa, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali zilizopo.

**Jitihada za Tume**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilianza jitihada za kupambana na matukio ya mauaji na vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi mnamo mwaka 2009 ilipofanya utafiti na uchunguzi katika maeneo mbalimbali nchini katika kanda ya ziwa na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na suala hili zima. Utafiti ulifanyika katika mikoa ya kanda ya ziwa Victoria na katika mkoa wa Mbeya ukihusisha jumla ya wilaya 16 ambazo ni Misenyi, Muleba, Biharamulo, Ngara, Geita, Sengerema, Kwimba, Magu, Misungwi, Bukombe, Kahama, Bariadi, Bunda, Musoma, Mbarali na Mbozi. Utafiti na uchunguzi huo pia uliangalia tatizo la mauaji ya vikongwe na suala la uchunaji ngozi za binadamu**.** Tutapata wasaa muda mfupi ujao kusikia kwa ufupi yale ambayo Tume iliyabaini.

Tume ilitoa mapendekezo mbalimbali, mengine tunadhani bado yanahitaji kufanyiwa kazi. Afisa mwandamizi wa Tume ataeleza zaidi kuhusu nini kilifanyika na changamoto zilizojitokeza.

Ndugu zangu, naomba kusisitiza kwamba mkutano huu ni fursa nzuri kwetu kulitazama tatizo hili kwa mapana na marefu, na kwa undani tupate muafaka wa jinsi ya kufanya kazi hii kwa pamoja.

**Ndugu washiriki,**

Naomba nimalizie kwa kuwaomba wadau wote kutoka Serikali, Asasi za Kiraia, viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali kutoa ushauri na ushirikiano kwa Tume na vyombo vingine vya Serikali kufanikisha mkakakati huo wa kutoa elimu kwa umma na hatimaye kukomesha mauaji na vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Mwalimu Nyerere alituambia "ukificha ugonjwa mauti yatakuumbua." Nami nasema, tuache kulionea aibu janga hili, ili tushinde vita hii.

Nawashukuru sana kwa kufika kwenu katika kikao hiki na nawatakia ushiriki mzuri ili hatimaye tuweze kufikia lengo letu la kuwalinda na kuwapa haki sawa watu wenye ulemavu wa ngozi Tanzania.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**